# STD 7 MID TERM 3 EXAM 2019

## KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* 1 *mpaka* 15. *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Maneno ya mzazi huyo ____**1**____ sana alipodai kuwa mtoto wake asome, asisome. ____**2**____ ni ____**3**____ tu. Matamshi hayo ____**4**____ ukosefu wa ____**5**____ kwa mzazi. Sikuelewa kwa nini akose ____**6**____ masilahi ya mwanawe.

Niliamua kumshauri ____**7**____ nikizingatia ya Wahenga kuwa ____**8**____.

**1.** A. imeshtusha B. ilishangaza C. yalishangaza D. alishangaza

**2.** A. kwao B. kwetu C. kwako D. kwake

**3.** A. moja B. mamoja C. njema D. mzuri

**4.** A. yalionyesha B. ilionyesha C. walionyesha D. alionyesha

**5.** A. heshima B. utajiri C. umaskini D. uwajibikaji

**6.** A. kubeza B. kudai C. kujali D. kutojali

**7.** A. kwa B. huku C. kama D. sana

**8.** A. Mtoto mkanye angali mdogo B. Mtoto akililia wembe mpe C. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo D. Mtoto mwerevu hafunzwi adabu

Michezo ni ____**9**____ burudani muhimu duniani kufuatia mapato ____**10**____ yanayotokana ____**11**____. Haya yanaweza ____**12**____ kwa mali ____**13**____ wanayopata wanaspoti hawa ____**14**____ kwenye riadha, soka, uendeshaji magari na michezo ____**15**____.

**9.** A. mighairi B. dhidi ya C. miongoni mwa D. licha ya

**10.** A. mingi B. mengi C. nyingi D. jingi

**11.** A. naye B. nalo C. nazo D. nayo

**12.** A. kuthibitika B. kudhibitishwa C. kuthibitishwa D. kuthibitika

**13.** A. nyingi B. mingi C. mengi D. wengi

**14.** A. wawe B. yawe C. iwe D. ziwe

**15.** A. nyingineyo B. nyinginezo C. mingineo D. mingineyo

*Kuanzia swali la* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo.*

**16.** Chagua kikundi chenye nomino za kawaida.
- A. Shungi, thureya, genge, kaumu.
- B. Nairobi, Maria, uhabeshi, tita.
- C. Gari, meza, kalamu, simu.
- D. Wema, upendo, furaha, uzito.

**17.** Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigiliwa mstari.
Mwanafunzi <u>mwerevu</u> hutuzwa <u>mara nyingi.</u>
- A. sifa, kivumishi
- B. kivumishi, kielezi
- C. kielezi, kivumishi
- D. kimilikishi, kiashiria

**18.** Mahali anapofungiwa mshukiwa akingoja kesi kumalizika ni,

| | |
|---|---|
| A. rumande. | B. kizimba. |
| C. gerezani. | D. korokoroni. |

**19.** Chagua wingi wa sentensi hii:
Rubani hakujua kuwa ningemsalimia.
- A. Rubani hawangejua kuwa tungewasalimia.
- B. Rubani hawakujua kuwa tungewasalimia.
- C. Marubani hawakujua kuwa tungemsalimia.
- D. Marubani hawakujua kuwa tungewasalimia.

**20.** Nomino **'ulezi'** inapatikana katika ngeli ya

| | |
|---|---|
| A. U - YA | B. U - ZI |
| C. U - U | D. U - I |

**21.** Chagua **kihusishi** katika sentensi ifuatayo.
Mgeni alisimama kando ya mjomba wangu.

| | |
|---|---|
| A. alisimama | B. mjomba |
| C. kando ya | D. wangu |

**22.** Chagua methali isiyo na maana sawa na **"siku za mwizi ni arubaini"**
- A. Ujanja wa nyani huishia jangwani.
- B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
- C. Mbio za sakafuni huishia ukingoni.
- D. Ndege mjanja hunaswa na tunda ukingoni.

**23.** Mke wa mjomba huitwa,
- A. shemeji.
- B. mkwe.
- C. mwanyumba.
- D. mkazahau.

**24.** Ni sentensi ipi iliyotumia **'kwa'** ya umilikaji?
- A. Aliadhibiwa kwa kuchelewa shuleni.
- B. Tulifika kwa shangazi jana jioni.
- C. Wageni wengi wamefika kwake leo.
- D. Nilikula wali kwa nyama jana.

**25.** Tegua kitendawili:
Bubu sema!
- A. upepo
- B. kiziwi
- C. kitabu
- D. kalamu

**26.** Kanusha:
Angelika angekuja angenikuta.
- A. Angelika angekuja hasingenikuta.
- B. Angelika asingalikuja asingalinikuta.
- C. Angelika hangekuja hangenikuta.
- D. Angelika asingekuja asingenikuta.

**27.** Chagua mapambo ya pua.
- A. Kipuli na kipini.
- B. Kipini na kishaufu.
- C. Herini na kishaufu.
- D. Kipuli na herini.

**28.** Jumla ya miaka mia moja ni,
- A. miteni.
- B. mwongo.
- C. karne.
- D. kikwi.

**29.** Chagua ipi si maana ya neno **'shinda'**
- A. Kaa mchana kutwa.
- B. Bila kujaa.
- C. Kuwa wa kwanza.
- D. Kaa usiku kucha.

**30.** Ni sentensi ipi iliyo katika **hali timilifu**?
- A. Amefika leo asubuhi kutoka mjini.
- B. Alifika leo asubuhi kutoka mjini.
- C. Angefika leo asubuhi kutoka mjini.
- D. Atafika leo asubuhi kutoka mjini.

*Soma taarifa ifuatayo kwa makini kisha ujibu maswali* **31 – 40**

Machoni pa wanakijiji wengi, mwendazake baba yangu alikuwa maskini hohehahe. Wengine hata walimwita mlofa. Kwangu binafsi, baba alikuwa tajiri licha ya kuwa mtule. Baba alikuwa maskini wa mali. Kazi yake ya kusuka vikapu ilikuwa ya kijungu jiko na ya msimu. Licha ya yote hayo, ni kazi aliyoifanya kwa moyo wa kujitolea. Aliienzi. Ndiyo aliyotulisha na kutuvisha.

Machoni na akilini mwangu, baba hakuwa maskini. Alikuwa chimbuko la hekima. Alikuwa mbegu ya ufanisi katika maisha yangu. La kushangaza sana ni kuwa, kinyume na mama yangu, baba hakunisisitizia sana ufanisi wa kupata kitu. Alipenda sana nifanikiwe kuishi na walimwengu kwa upendo na amani. La msingi sana lilikuwa umuhimu wa kusaidia waliohitaji msaada wangu.

Jioni moja, alinisikia nikimweleza ndugu yangu jinsi nilivyokataa kumsaidia mwenzangu darasani. Mwenzangu huyo aliudhika sana kwa tabia yangu ya ubinafsi. Hakuchelewa kuniita. Pindi nilipoenda alipokuwa akiota moto huku akichoma ndizi. Alinituma niende dukani ninunue mishumaa miwili. Hilo nalo lilinitisha si haba.

Niliileta mishumaa na kunyamaa jii kama kaburi ili nione lile ambalo lingejiri. Baba aliuwasha mshumaa mmoja. Mwangaza haukujaa chumbani mote. Baadaye aliniambia niutumie mshumaa huo kuuwasha ule wa pili. Nilifanya hayo huku nikitetemeka. Baba alinikazia macho huku akitabasamu. Akaniuliza iwapo palikuwa na tofauti. Nilimjibu kuwa chumbani mlikuwa na mwangaza zaidi kuliko hapo awali. Mlipendeza zaidi.

Bado baba akanikazia macho akaniuliza iwapo mshumaa wa kwanza uliathirika kwa kuuwasha ule wa pili. Nilijibu, "La, haukuathirika kwa vyovyote vile." Basi mwanangu, ukiwa na uwezo na fursa, wasaidie wenzio. Hutapoteza chochote kwa kufanya hivyo bali utawapa uwezo wa kujitegemea na bila shaka ulimwengu utakuwa mahali bora zaidi pa kuishi.

Kama ulivyoona, mshumaa unaowaka haupotezi chochote kwa kuuwasha ule mwingine. Nawe pia hutapoteza chochote kwa kuwasaidia wenzio. Mishumaa miwili imeleta mwangaza zaidi chumbani. Vivyo hivyo, mkiwa wengi, mnaojua , mtaleta maendeleo mengi duniani. Tafadhali usiwe mchoyo wa hekima. Wasaidie wengine uwezapo kwani uwezo huo umetunukiwa na mola

Maneno yake baba yalinibadilisha kwa kiwango kikubwa sana. Nikawa mtu wa kuwasaidia wahitajio msaada.

Kumbe Walimwengu ni kusaidiana na watu ni kikoa. Hata hivyo, ukarimu usizidi uwezo.

**31.** Je, kwa nini baadhi ya wanakijiji walimwita babaye msimulizi mlofa?
A. Walimdharau kutokana na tabia zake.
B. Walimdharau kutokana na hali yake.
C. Alikuwa na mazoea ya kunywa pombe.
D. Alikuwa na mazoea ya kuwashauri wenzake.

**32.** Msimulizi alimwona babaye kuwa,
A. mzazi mkali.
B. maskini wa mali.
C. mzazi wa kawaida tu.
D. kielelezo mwafaka maishani mwake.

**33.** Ni kweli kusema kuwa kazi ya mzazi wa msimulizi,
A. ilikuwa haramu.
B. ilitegemea nyakati.
C. ilikuwa ya pato la wastani.
D. ilikuwa ya kulazimishwa.

**34.** Ni jambo lipi ambalo baba mtu alithamini zaidi?
A. Fadhila.
B. Nidhamu.
C. Urafiki.
D. Amani.

**35.** Ni lipi ambalo lilimfanya baba wa msimulizi amshauri katika siku husika?
A. Ubahili wa msimulizi.
B. Hekima ya babaye msimulizi.
C. Mazoea ya baba yake.
D. Ukarimu wa msimulizi.

**36.** Kwa nini msimulizi alishtuka alipotumwa aende akanunue mshumaa?
A. Alihofia kuchomwa.
B. Babaye alikuwa na hasira.
C. Hakuelewa lengo la babaye.
D. Msimulizi aliogopa mshumaa.

**37.** Ni kweli kusema,
A. babaye alikuwa msomi.
B. msimulizi aliuwasha mshumaa.
C. msimulizi alikashifiwa na nduguye.
D. msimulizi alikuwa hodari katika hesabu.

**38.** Kilichosababisha babaye kutabasamu ni,
A. alitaka msimulizi awe na ujasiri wa kuwasha mshumaa.
B. alifurahishwa na mwanawe.
C. alitaka mwanawe atabasamu.
D. kufurahia mwanga wa mshumaa.

**39.** Funzo kwa msimulizi ni,
A. awasaidie tu marafiki zake.
B. anapowasaidia wenzake pia ajisaidie.
C. asikubali msaada wa wengine.
D. asisaidie kupita uwezo wake.

**40.** Methali inayofaa kifungu hiki ni,
A. Wengi wape.
B. Penye nia pana njia.
C. Kuishi kwingi ni kuona mengi.
D. Jungu kuu halikosi ukoko.

*Soma ufahamu ufuatao kwa makini kisha ujibu maswali* **41 – 50**

Nilipokuwa katika shule ya msingi, nilikuwa maarufu sana kitongojini petu. Weledi wa lugha walisema nilikuwa maarufu kama usingizi wa usiku.

Enzi hizo, kiwango cha elimu Kariani petu kilikuwa cha chini. Ikizingatiwa kuwa mimi tayari nilikuwa katika darasa la tano, na fauka ya hayo tabia zangu ziliwavutia wengi. Nilikuwa na hulka ya ukarimu. Nilijipata nikiandamwa na wengi. Kisa na maana, niwasomee nyaraka walizokuwa wakitumiwa na ndugu na marafiki zao. Mara kwa mara nilihitajika hata kuzijibu nyaraka hizo. Machoni pao nilikuwa msomi.

Wazazi wengi walinifuata niwasomee barua walizozipokea kutoka kwa jamaa zao mjini. Wengine waliniita nisome barua kutoka kwa wapenzi wao walioishi maeneo mbalimbali nchini. Walipendezwa na hulka zangu za kutotangaza yale niliyoyasoma. Huduma zangu zilifuatwa na tuzo za kila aina kuanzia vyakula na asusa kama vile keki hadi pipi. Miaka michache baadaye, nilihama kijijini kwenda kujitafutia riziki. Si waambao waliamba riziki ya mbwa i miguuni mwako! Kutokana na pandashuka za maisha nilizamia lulu mjini.

Juzi niliporejea kijijini kuwajulia hali ndugu na jamaa msimu wa Noeli, niliwaza kulinganisha hali ya sasa na ya zamani. Nilipata mambo yamebadilika si haba! Wengi wa wanakijiji kinyume na hapo awali wameikumbatia elimu. Baadhi ya waliozitegemea huduma zangu leo hii wanajitegemea.

Walijiunga na elimu ya ngumbaru. Teknolojia ya mawasiliano imeimarika vilivyo kijijini. Karibu kila mwanaKaria ana rukono. Nilitarajia njia ya mhadithi iwe hafifu lakini nilikuwa nimekosea. Mawasiliano ni bora na imara zaidi.

Mshangao wangu ukazidi nilipoona kuwa wengi walitumia rununu kwa shughuli zao mbalimbali kama vile kulipia bili zao, kufuatilia shughuli katika soko la hisa na soko la bidhaa za kilimo. Nilipotalii soko la kwetu nilikumbana na mabadiliko yaliyonifanya bubu.

Vijumba vingi ambavyo hapo awali vilikuwa vya kupikia na kuuzia supu vilikuwa vimegeuzwa na kuwa vya mawasiliano ya wavuti. Wananchi tele, vijana kwa wazee walifurika pale kupata huduma za mdahalishi kama vile baruapepe. Nikazikumbuka siku za hapo nyuma.

Nikaelewa kuwa kiteknolojia, tumepiga hatua za kutambulika. Hatua ambayo imerahisisha na kuboresha mengi. Zamani tulikuwa gizani. Kweli ulimwengu umegeuka kuwa kijiji kimoja. Nacho kijiji cha kwetu hakijaachwa nyuma.

**41.** Akiwa shuleni, umaarufu wa msimulizi ulitokana na.
A. elimu yake ya juu.
B. uwezo wake wa kuandika na kusoma barua.
C. kuzawadiwa kusoma wala kuandika kati ya wengine.
D. kutojua kusoma wala kuandika kati ya wanakijiji.

**42.** Tabia zilizowavutia wanakijiji ni.
A. usiri wake.
B. usomaji wa barua.
C. huruma yake.
D. unyamavu wake.

**43.** Ni jambo lipi lililosababisha msimulizi kuhama kijijini?
A. Kuendelea na masomo.
B. Kujenga nyumba na kununua shamba.
C. kujitafutia maisha.
D. Kazi ya kusoma barua ilikuwa imechosha.

**44.** Kulingana na kifungu hiki ni mambo yapi aliyoyapata msimulizi aliporudi kijijini?
A. Shule nyingi kujengwa.
B. Maduka yote yaliyokuwa yamefungwa.
C. Wanakijiji wote kumiliki rununu.
D. watu wengi wameongeza kiwango cha elimu.

**45.** Ni neno lipi si kisawe cha kijiji?
A. Karia.
B. Soko.
C. Kiambo.
D. Kitongoji.

**46.** Baada ya kurejea kijijini, msimulizi alitarajia yapi?
A. Watu wawe wametaabika.
B. Watu wengi wawe wametajirika.
C. Biashara nyingi ziwe zimeimarika.
D. Mawasiliano ya simu yawe na shida kubwa.

**47.** Ni ipi kati ya njia hizi si ya mawasiliano?
A. Rukono.
B. Baruapepe.
C. Televisheni.
D. Garimoshi.

**48.** Kulingana na taarifa hii, ni kina nani wamekumbatia maendeleo pale kijiji?
A. Wasomi pekee.
B. Matajiri pekee.
C. Watu wa kila sampuli.
D. Vijana pekee.

**49.** "Zamani tulikuwa gizani," msimulizi anaongea kuhusu zama zipi?
A. Kabla hajarudi kijijini.
B. Kabla kuja kwa elimu.
C. Kabla kuja kwa teknolojia.
D. Alipokuwa mwanafunzi kijijini.

**50.** Kifungu hiki hakionyeshi faida za.
A. elimu.
B. teknolojia.
C. kusaidia.
D. kwenda mjini.